# KUSTAHIMILI MATESO NA TAABU NYINGI WALIZOPITIA MITUME NA MANABII NA WATAKATIFU WOTE WALIOTUTANGULIA KULITEGEMEA SANA NGUVU ZA ROHONI WALIZOKUWA NAZO.

**MAANDIKO: Mith. 24: 10, Yoh. 20: 19 – 23, Mdo. 2: 1 – 4**

1. **UTANGULIZI:**
   Maana ya kustahimili ni **kuvumilia**. Yaani mteule anakuwa na uwezo wa kusimama imara bila kutikisika au kuogopa na bila kukata tamaa kabisa wakati anapopitia katika majaribu mazito ya mwili na dhiki pamoja na vita vikali mfano wa Stephano. ***Mdo. 7: 54-60.***

- **Maana ya kuvumilia Kibiblia:-**Ni ule uwezo wa ndani ya moyo wa mtu wa Mungu **unaomwezesha** kuchukuliana na hali ngumu anazokutana nazo katika safari hii nzuri ya wokovu aliyoianza baada ya kuokoka pasipo kulalamika (kunungunika)
- Roho Mtakatifu pale tunapompokea Yesu Kristo kama Bwana na Mwokozi wetu; yeye huingia ndani yetu na kutuwekea tabia kama aliyokuwa nayo Yesu mwenyewe ili **kutuwezesha** kuchukuliana na hali zozote ngumu pamoja na majaribu mbalimbali tunayokutana nayo pasipo kulalamika wala kukata tamaa kabisa.
- Wakati watu wengine wanakuonea huruma; wewe Roho Mtakatifu anakupa ufahamu wa hali ya juu wa kuona furaha iliyo nyuma ya changamoto unayopitia jambo ambalo linakutia moyo wa kusonga mbele pasipo kulalamika wala kunung'unika. ***Ebr. 12: 1 -3.***
- Ni kama mgonjwa saa ya kutundikiwa drip na daktari, ni kweli sindano inauma sana, lakini kwa sababu anajua kwamba hiyo ndiyo njia ya uponyaji wake, anavumilia

hata kama ni drip kumi pasipo kunung'unika; na inapoisha, na daktari akachelewa kumwekea nyingine, mgonjwa mwenyewe **anadai!!**

- Ni kama pia mwanamke na kubeba mimba na kujifungua mtoto!!! Hiki huwa ni kipindi kigumu sana kwa mwanamke; usingetegemea kumwona mwanamke huyu huyu aliyekuwa kama kituko kwa ujauzito wake kubeba mimba tena ndani ya kipindi cha miaka 2 tu au hata chini yake!!! Siri yao ni nini hasa!! Ndani ya kila mwanamke Mungu ameweka uwezo unaowawezesha kuvumilia hali hiyo pasipo kulalamika kwa sababu ya furaha watakayoipata baadae. **Yoh. 16: 20 -21.**
- Kwa hiyo Roho Mtakatifu anapokaa ndani ya mtoto wa Mungu, kazi yake ni kumfunua Yesu Kristo na uzuri wake ndani ya mteule huyo; na hata badaae mteule atakapokuwa anapitia dhiki na changamoto nyingine nyingi; yeye hazioni hizo changamoto kama kikwazo, yeye anaona na kukaza macho yake kwenye furaha inayomngoja baada ya taabu hiyo kupita na hivyo kumfanya asikate tamaa kamwe wala kulalamika. **Mdo. 7: 54 – 60,**
  **Mwanzo 45: 1 -15.**

***Note*: Kustahimili (kuvumilia) ndicho kipimo cha Mungu wetu cha imani yetu kwake; ndicho kipimo cha huduma zetu zote kwake, ndicho kipimo cha upendo wetu kwake, na bila kuwa na tabia ya uvumilivu na kufurahi wakati tunapopitia majaribu mbalimbali kwa ajili ya Jina lake, siyo rahisi tukashuhudia uzuri wake kamili wala baraka zake za kushangaza zikimwagwa juu yetu. Yak. 1: 2 – 4**

- Yesu akasema "**Ulimwenguni mnayo dhiki, lakini jipeni moyo mimi nimeushinda Ulimwengu"** maana yake ni hii "mtu aliye na uwezo wa kujipa moyo saa anapitia katika dhiki za Ulimwengu huu ni yule aliye na uwezo wa kukaza macho yake kwa Yesu na uzuri wake wa ajabu unao mngoja baada ya kuvuka jaribu hilo kuliko kupoteza muda akitazama ukubwa wa jaribu na kulitafakari jambo ambalo litamfanya aishie kulalamika na kukata tamaa **Yoh. 16: 33, Filip. 2: 5 – 11, Mith. 24:10. Kiasi cha nguvu za Roho Mtakatifu zilizojaa ndani ya mtu wa Mungu ndicho kitakachomwezesha kuvuka salama na ushindi katika kila jaribu atakalokutana nalo**.

2. **ASILI YA NGUVU ZA MUNGU NDANI YA MWANAFUNZI WA YESU. Yoh. 20: 19 -23, Mdo. 1: 5, 8, 2: 1 -4, Yoel. 2: 28 – 29.** Yesu kabla ya kuondoka na kurudi juu kwa Baba baada ya kazi ya Ukombozi kukamilika; aliwatokea wanafunzi wake wale waliokuwa wamejaa hofu na waoga hata ingawa alikuwa ametembea nao muda wa **miaka 3$^1/_2$** na kuwafundisha mengi na **akawavuvia** na kisha akawaambia wampokee Roho Mtakatifu (**Emphusao).**

- Kama tulivyo angalia maana ya **Emphusao kuwa ni kuwafanya sasa wanafunzi wake kuwa hai kiroho kama ambavyo Mungu alipompulizia Adamu pumzi ya uhai puani mwake Adamu akawa nafsi hai**- ***Mwaz. 2:7.***

- **Asili ya nguvu za Mungu ndani ya Wanafunzi wa Yesu ni Roho Mtakatifu waliyempokea**.
- Kumbuka kwamba, pamoja na Yesu kutembea na Wanafunzi hawa **miaka 3$^1/_2$** na kuwafundisha mengi na kuomba nao, na hata wao wenyewe kutoa pepo na kupoza wagonjwa, kabla ya kuvuviwa na Bwana Yesu

**(Emphusao**) ili wampokee Roho Mtakatifu bado walijaa woga, walikuwa ni watu wa mwilini tu ambao saa ya majaribu walikata masikio ya adui zao kwa kutumia panga zao (yaani mtu anakwenda kwenye maombi amebeba na upanga!! **Luk. 22: 47 – 51 (Yoh. 18: 3 – 11)** hadi wakati huu kabla ya kuvuviwa ( kufanywa hai kiroho) walikuwa wanamfuata Yesu kwa mtindo wa wafuasi wa **Agano la Kale. – 2Kor. 3: 12 – 18** (Fikira zao zilikuwa zimetiwa uzito na ufahamu wao kuhusu Yesu na Ukuu wake na uzuri wake wote nao ulikuwa umefungwa wasifunuliwe kabisa hadi Roho Mtakatifu watakayempokea atakapowafunulia baada ya Yesu Kristo kuondoka. **Yoh. 16: 12 – 15** (Hata ingawa siku moja Yesu alijifunua kwa wachache Mlimani, bado wao walilichukua jambo hili kimwili maadamu ufunuo dhahiri wa kiroho ili wamjue Yesu Kristo kwa kina bado ulikuwa haujawatokea maadamu walikuwa hawajavuviwa ili wampokee Roho Mtakatifu ambaye ndiye anayemfunua Yesu halisi ndani yetu. ***Math. 17: 1 – 9.***

- **Roho Mtakatifu ndiye nguvu yetu pekee iliyo na uwezo wa kutusaidia kuvumilia dhiki zetu zote kama alivyomsaidia Yesu kuvumilia dhiki na mateso mbalimbali- *Luk. 4: 1 – 14,* na mteule yeyote ambaye hajajazwa Roho Mtakatifu ni sawa na mtoto yatima hata sasa**. **Yoh. 14: 16 – 18, 16: 7.**

NB: Ndiyo sababu katika Agano la Kale – watu washuhuri (Makuhani, Manabii na hata Wafalme) walikuwa wanamiminiwa mafuta kichwani kama ishara ya kupata nguvu za Mungu zitakazowasaidia kumtumikia Mungu na kukabiliana na kila aina ya hatari itakayojitokeza mbele yao. ***Kut. 30: 22-30, 1Samwl. 9: 22 – 27, 10: 1-9, 16: 1, 12- 13, 1Wafal. 19: 15 – 21.***

- **Yesu alimkabidhi Roho Mtakatifu Kanisa alilolinunua kwa gharama kubwa ili ahakikishe linakuwa na nguvu na linafika Mbinguni, Kanisa linaloshinda ulimwengu kama yeye alivyoshinda; Ni hatari sana tena sana kukaa ndani ya Kanisa bila kuvuviwa (kufanywa hai kiroho kwanza) ili umpokee Roho Mtakatifu ambaye ndiye nguvu yetu na kiongozi wetu.)**

- **Kumbuka kutoona umuhimu wa kujazwa Roho Mtakatifu na ukampa nafasi ya kwanza katika Maisha haya ya wokovu, maisha yako ya kiroho yatakuwa makavu daima na yasiyo na mwelekeo wowote na kamwe hutapenya wakati utakapokabiliana na dhiki ambayo kila mmoja lazima apitie (utazimia tu). ukijikuta unaishi kwa huzuni tu wakati wote, wakati unasema umeokoka, umejaa mahangaiko, unaona wokovu kama mzigo mzito usiokupa furaha basi elewa hujavuviwa, (hujafanywa hai kiroho) na siyo rahisi Roho Mtakatifu aje kukaa ndani yako.**

3. <u>Kazi za Roho Mtakatifu ndani ya Mwamini</u>
    a. **Kazi ya kwanza iliyo kubwa na muhimu sana ni kuumba tabia za Kiungu kwanza ndani ya mwamini. 2Petr. 1: 3 – 4.** Kabla ya kuokoka; kila mtu anakuwa na tabia zake nyingi za kimwili; Roho Mtakatifu kazi yake ni kushika hatamu kwanza kwa mwamini; kumfanya awe hai kiroho na kufisha matakwa ya kwanza ya mwili wake na hivyo kumwezesha kuanza kuishi maisha matakatifu. **Galat. 5: 16 – 25.**

- **Hakuna mtu anayeweza kuishi maisha matakatifu bila kujazwa na Roho Mtakatifu. Lazima awe na Roho Mtakatifu ambaye ndiye mzalishaji mkuu wa tunda la Roho ndani yetu, na kazi ya tunda la Roho ni kuumba sasa tabia za Mungu ndani ya mteule. 1Kor. 3:1 – 3.** Vinginevyo tutakaa ndani ya wokovu (Kanisani tukiwa tumejaa tabia za mwilini (za woga, za visasi, za chuki, n.k**.) 1Kor. 2: 10-16.**

b. **Kazi ya pili muhimu sana ni pale Roho Mtakatifu anapotupa akili ya Kiungu na ufahamu mwingine tofauti na akili na ufahamu tuliokuwa tumepewa na Ulimwengu huu. *2Timoth 2:7.*** Roho Mtakatifu anakuwa mwalimu wa kutufundisha mambo. ***Yoh. 14: 26*** na kukupa maarifa yatakayoshangaza wengi waliotufahamu huko nyuma. **Mdo. 4: 13 – 14**
   - Eneo hili la Roho Mtakatifu kuwapa wateule wa Mungu akili ya Kiungu na ufahamu wa hali ya juu katika mambo mbalimbali hata kama ni maswala ya ujuzi wa kazi mbalimbali bado kizazi cha leo hakilifaidi sana. **Dan. 1: 17- 21, Mwanz. 41: 25 – 46, Kut. 31: 1 – 5.**

c. **Kazi ya tatu ya ajabu mno ni pale Roho Mtakatifu anapotupa nguvu ya kuhubiri/kufundisha injili iliyojaa uweza wa kugeuza mioyo ya watu na wanauacha uovu kabisa na kumwelekea Mungu wa kweli. Mdo. 1:8, Mdo. 6: 7 – 10, 17: 5 – 6**. Kama Yesu alivyowashangaza wakuu wa dini kwa mafundisho yaliyojaa uzima wa Mungu. **Luk. 4: 16 – 22, ndivyo na Injili yetu leo itakavyoendelea kuwashangaza wengi endapo tu itatoka kwa mtumishi aliyejaa nguvu za Roho Mtakatifu.**

- Mtu kuacha dhambi kama **ulevi, uzinzi, uongo, rushwa; ufisadi, chuki, wivu, kuacha mila yake, dini yake, kuacha ushirikina na mambo mengine yaliyokuwa yanampa faida ya kimwili siyo jambo la kawaida, ni mpaka akutane na injili inayotoka katika moyo uliojaa nguvu za Roho Mtakatifu tu**!!!
- Pepo kutoka ndani ya mtu siyo mchezo, ni pale tu anapokemewa na Mtumishi aliyejaa nguvu za Roho Mtakatifu, vinginevyo hatoki. **Mdo. 19: 13 – 16.** Roho Mtakatifu ndiye anayezalisha karama za ajabu mno ndani ya moyo wa mtumishi wa Mungu na kumwezesha kufanya huduma za ajabu zisizowezekana kwa akili ya kibinadamu. **1Kor. 12: 4 -11, 28.**

d. **Kazi ya nne iliyo maalumu sana ni kutupa furaha na ushindi wakati tunapokuwa tunapitia katika dhiki na majaribu mbalimbali**. **Mdo**. **5: 40-42 na Mdo. 16: 16 – 26**. Huwezi kuimba nyimbo za kumsifu Mungu wakati unapitia dhiki na taabu na mapigo kama hujajaa nguvu za Roho Mtakatifu; na wala huwezi kuwa jasiri tena na furaha tele wakati unakabiliwa na kutupwa katika tanuru la moto kwa sababu umekataa kusujudia sanamu. **Dan. 3: 8 – 23, 6: 4 – 17.** Lazima tu utafikirifikiri namna gani ufanye ili kuepuka hali hizo. Lakini kama umejaa Roho Mtakatifu; na uu hai kiroho, wakati unaonewa na kuteswa saa hiyo ndipo wimbo mpya unaimbika. **Luk. 12: 8 – 12.**

e. **Kazi nyingine kabambe ya Roho Mtakatifu ni kutuongoza na kututia kwenye kweli yote. Yoh. 16: 13, Rum. 8:14, Isaya 35: 8. Swala la mtu kuongozwa haliepukiki, iwe ni Nchi lazima iwe na kiongozi, liwe ni shirika lazima liwe na kiongozi, liwe ni jeshi lazima liwe na kiongozi, liwe ni**

**Kanisa lazima liwe na kiongozi, iwe ni ndoa lazima iwe na kiongozi, nchi ambazo hazina viongozi zimejaa machafuko tupu!! Ndivyo ilivyo katika safari nzuri ya wokovu ya kwenda juu Mbinguni kwa Baba; Roho Mtakatifu ni kiongozi wetu makini atakayehakikisha tunafika salama.**

- Kama tutamsikiliza hasa, hatutapotea kamwe. **Mdo. 16: 6 – 12.**
- Atatuongoza hata katika eneo la kuoa/kuolewa. **Mwanz. 24: 10 – 27.**

***Note:*****Kiongozi siku zote anajua anakotaka watu wake wafike, anaijua njia yote na daima anakuwa ametangulia mbele yao; kazi ya wanaoongozwa ni kumsikiliza tu. Kut. 23: 20 – 23. Malaika wa Bwana ni Mungu mwenyewe, (Roho Mtakatifu ni nafsi ya tatu ya Mungu (Baba, Mwana na Roho Mtakatifu).**

f. **Kazi nyingine nyeti sana ni kutupasha habari za mambo yajayo. Yoh.16:13, 2Wafal. 6: 8-12, Amos. 3: 7, Zab. 25: 14.** Yesu hakutaka watumishi wake watembee kama vipofu gizani, akamtoa Roho Mtakatifu ambaye atawajulisha mambo ya sasa na yajayo!!! Neema hii hawana wanadamu wa kawaida wala Wafalme wa Ulimwengu huu; wamejaliwa watoto wa Mungu tu na Roho Mtakatifu. **Math. 13: 10-11.**

- Yohana Mtakatifu alipojulishwa habari ya mambo yajayo alizimia kabisa. **Ufun. 1: 9 – 20**
- Nuhu alipojulishwa habari za mambo yajayo, hakudanganyika ngo!!! **Mwanzo 6: 13 – 22.**
- Ibrahimu alipojulishwa habari za mambo ya Sodoma na Gomora, aliomba sana**. Mwz. 18: 16 – 33**

- **Leo hii tunasukumwa sisi wateule katika maswala ya Ibada na kuwafundisha watoto wetu kweli ya neno la Mungu na hata kuja kwenye mikesha, kutoa zaka na sadaka nzuri n.k. sababu hatuna habari hasa ya nini kinachokwenda kuupata Ulimwengu huu baada ya Yesu kulinyakua Kanisa lake. Ufun. 16: 1 – 21.**

g. **Kazi nyingine nzito ya Roho Mtakatifu ndani yetu ni kuomba maombi ya kuugua, maombi ya kuzama, maombi ya kina na yasiyo na ubinafsi. Rumi. 8: 26 – 27, 1Samwl. 1: 10 – 17.** Swala la maombi ya kuugua, maombi ya kuzama kwa kina kabisa haliwezekani kwa mtu anayeomba kwa akili zake tu; bali linawezekana kwa mtu anayeomba katika roho akitawaliwa na Roho Mtakatifu. **Neh. 1: 4 – (Math. 26: 36 – 44, Luk. 22: 40 – 46)**

- Kama kuna vitabu vingi ambavyo vimeandikwa na watumishi wengi wa Mungu duniani, basi ni vitabu vya maombi; maombi ni eneo lililo na upinzani mkubwa sana kwa wateule wa Mungu maana mwombaji halisi lazima atajulishwa na kuonyeshwa mambo mengi na Mungu na ataharibu mikakati mingi ya ibilisi; bila Roho Mtakatifu kupewa nafasi saa ya maombi, huwezi kuomba hata saa moja bila kulala usingizi!!
- Ni Roho Mtakatifu tu aliyemsaidia hata ndugu yetu Paulo pale alipokabiliana na udhaifu katika eneo la maombi yake; alipomruhusu Roho Mtakatifu, akajikuta ameomba kwa kuugua na kwa kuzama hadi akashindwa kuelezea!!! **Rum. 8: 26 – 27**
- **Hakuna bingwa wala mwalimu hasa wa somo la maombi pamoja kuwa na waandishi wengi; bingwa wa maombi ni Roho Mtakatifu ambaye anajua na anaweza kutuombea kama anavyotaka Mungu. 1Samwl. 1: 10 – 16, 1Kor. 14: 2 – 4.**

h. **Kazi nyingine ya ajabu na ya miujiza kabisa ya Roho Mtakatifu ni pale anapoihuisisha miili yetu hii iliyokuwa katika hali ya kufa; iliyokuwa imechoka na kuchakaa. Rumi 8: 11 (He who raised up Christ Jesus from the dead will also (Restore) to life your mortal bodies through His Spirit who dwells in you.**

- **Neno Restore to life your Mortal bodies – lina maana ya kurudisha/kutengeneza/kuponya miili yetu hii ya kufa kupitia Roho Mtakatifu ambaye alitengeneza na kurudisha uhai katika mwili wake Bwana Yesu uliokuwa umekufa na ambao ulikuwa haufai kabisa. Yoh.20:19 – 22.**
- **Roho Mtakatifu ana kazi ya ajabu ya ku-restore/ kutengeneza/kuponya miili yetu hii iliyokuwa imechakazwa na shetani kwa mambo mengi.Mark.5:25-34. Roho Mtakatifu ndani yetu ni muumbaji, ni fundi wa kukarabati miili hii tuliyo nayo!!! Hili ni lengo na kusudi maalumu la Roho Mtakatifu kukaa ndani yetu. Atahuisha hata tumbo la uzazi lililokuwa limeharibiwa huko nyuma n.k.**

i. **Kazi nyingine iliyo ya kipekee sana ni ile ya kutuwezesha kumtukuza Yesu Kristo katika kiwango anachostahili kutokana na kazi kubwa ya ukombozi aliyoifanya pale msalabani**. **Yoh. 16: 14, Luk. 1: 46 – 55, 1Samwl. 2: 1 – 8, Zab. 103: 1 – 5, Yoh. 16: 14**, (**He will honor and glorify me")** Roho Mtakatifu ataanzisha hali ya mteule kumheshimu na kumwadhimisha Mungu moyoni mwake; atamsifu Yesu na kumwabudu na kumwinua kwa viwango vya hali ya juu sana pale anakumbuka kazi kubwa ya ukombozi ambayo Yesu amemtendea yeye ambaye hakustahili!!!

- **Furaha na shangwe zetu juu ya Yesu Kristo hazijaongezeka kwa sababu hatujamruhusu Roho Mtakatifu atupe ufunuo halisi juu ya kazi ambayo Yesu ameifanya katika maisha yetu**.
- Mariamu alimwadhimisha Mungu baada ya kuona kwamba Mungu amemchagua yeye asiyestahili kumzaa mwokozi wa Ulimwengu!!!! **Kuwa Mama wa kumzaa Mfalme Yesu siyo mchezo; ndiyo sababu wengine wanamwabudu leo.**
- Mfalme Daudi anaiambia nafsi yake isisahau kwamwe fadhili ambazo Bwana amemfanyia, lakini badala yake nafsi yake na vyote vilivyomo vimhimidi Mungu Daima!!!! **2Samwl. 6: 12 – 15 – anakumbuka Mungu alimtoa wapi ambako hata Baba yake mzazi alikuwa hamthamini. 1Samwl. 16: 11 – 13**
- Eneo hili la sifa (kumsifu na kumtukuza Mungu bado!!! Na ndiyo sababu hatuuoni utukufu wa Mungu ukifunika Hekalu lake!!! **2Nyak. 5: 1 – 14.** ( Hapa kuna mambo kadhaa ya kujifunza na waimbaji waliojitakasa.
- Vyombo vilipigwa kwa ustadi
- Waimbaji na wengine wote walikuwa kama mtu mmoja
- Kila mmoja alitoa sauti yake kwa nguvu ili kumwadhimisha Bwana kutokana na fadhili zake – Nini kilitokea - utukufu wa Bwana kushuka. **Soma hata Ezra;** Yeye alikuwa na Waimbaji (kwaya moja watu **128 (Ezra 2:41**).
- Daudi alikuwa na Kwaya kubwa ya **waimbaji 288** kwa ajili ya kumwadhimisha Mungu. **1Nyak. 25: 1 – 31.**

j. **Kazi nyingine ya kumi ni kuhakikisha wakati wote dhamiri ya mtoto wa Mungu iko hai. Rum. 2: 14 – 16**. Kazi kubwa aliyofanya shetani ya kwanza kwa Baba zetu wa kwanza ni kuua dhamiri zao kwanza. Na mtu ambaye dhamiri yake imekufa hana tofauti na mkoma; hata anapofanya dhambi hajisikii hatia moyoni tena!!! Roho Mtakatifu anapoingia moyoni mwangu na kunifanya kuwa hai kiroho; anaiamsha na dhamiri yangu ili iwe hai wakati wowote!!!! Ukitaka kugusa dhambi tu dhamiri inakuchoma hapo hapo ***– 1Samwl. 24: 1 – 8, 2Samwl. 24: 1 – 10.*** Dhamiri ya mtu ikifa, hata toba kwake ni ya kulazimisha kama Sauli. **1Samwl. 15: 1 – 30.**

- Ndiyo sababu Roho Mtakatifu ameachwa na Yesu Kristo kwa lengo la kuhakikisha dhambi ndani ya mtu; haki pamoja na hukumu. **Yoh. 16: 8 – 11.**

***Note:*** **Dhamiri ni hakimu asiyefichwa na chochote ndani ya mtu.**

4. **<u>Jinsi ya kujazwa na Roho Mtakatifu</u>**
    - Lazima mteule awe na **kiu** (awe na hamu yeye mwenyewe. **Yoh. 7: 37 – 39**. Katika eneo hili tunazidiwa hata na wachawi pamoja na waganga wa kienyeji!!! ***Mdo. 8: 14 – 24-*** **wao hupata hamu ya Roho Mtakatifu kiasi cha kuwa tayari kutoa fedha nyingi ili wampate.**

**<u>ROHO MTAKATIFU NI MFANO WA:-</u>**

a. Ni upepo – **Mdo. 2:2 - Humwoni lakini utaona kazi zake ndani yako**
b. Ni maji – **Yoh. 7:37 – 39- Atakuburudisha saa umechoshwa na majaribu**
c. Ni moto – **Mdo. 2:3 - Atateketeza hofu zote na kukufanya uwe hai kwa mambo ya Mungu**

d. Ni mafuta. **1Yoh. 2:27 - atakulainisha na kukufanya kuwa mnyenyekevu na Mtumishi wa watu na siyo Bwana**

e. Ni kama njiwa. **Math. 3:16 – 17 - atakuwezesha kusamehe Wote waliokuumiza na kuwapenda kwa dhati.**

**Tamani sana ndugu yangu Roho Mtakatifu kujazwa tena kwa kina kisichovukika ili yote niliyoyafundisha katika somo hili yawe halisi kwako.**

**Note:** Kuna watu Roho Mtakatifu kwao ni kama umande juu ya ardhi ambao hauwezi kuchipisha chochote!!!. **Mwanz. 2: 4 – 6.** Zipo mbegu chini ya ardhi yote; lakini haziwezi kudhupuswa na umande, zinahitaji mvua**!!!**

- **Tunatakiwa tujazwe Roho Mtakatifu hadi tuwe mto usiovukika tena. Ezek. 47: 1 – 5.**

**Bwana libariki Kanisa lako. Wimbo. Tenzi 12.**

***Na***
***Askofu Dr. L. Mwizarubi***
***May 2021***